GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. **244** R/Awwal-R/Akhir **1446** AH Oktoba– **2024** Tabook **1403** HS BEI TSH 800/=

RAIS SAMIA: AMANI NDIYO NGUZO YA MAENDELEO YA TAIFA LETU.

Na Rajabu Abasi Mkieti
Kitonga –Dar es Salaam



Mh. Mussa Zungu Mbunge na Naib Spika akihutubia kwa Niaba ya Rais Samia, katika mkutano wa Ahmadiyya - Kitonga

Serikali ya Tanzania imeitaka Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya nchini kuendelea kusimamia na kuhakikisha Amani inadumishwa na kulindwa kwa nguvu zote kwani ndio nguzo ya maendeleo ya nchi yetu. Wito huo wa Serikali umetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dokta Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Naibu Spika wa Bunge la Tanzania Mussa Zungu alipokuwa akimwakilisha Rais siku ya Septemba 28 mwaka huu katika Mkutano Mkuu wa 53 wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania yaani Jalsa salana uliofanyika katika jiji la Dar es salaam wilaya ya Ilala kata ya msongola Kitonga. Akizungumza baada ya kuhutubia katika mkutano huo



Mheshimiwa Mussa Zungu amesema Watanzania wote ni ndugu hivyo ni vyema kudumisha udugu huo kwa kulinda Amani ambapo Rais Dokta Samia amezitaka Taasisi mbalimbali ikiwemo za dini kuungana naye katika kuleta maandeleo. Akiizungumzia Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania Mheshimiwa Zungu amesema Serikali inatambua juhudi za Jumuiya ya Ahmadiyya nchini na hivyo inathamini Mchango unaotolewa katika masuala mbalimbali ikiwamo ya Kijamii kama Kujenga Shule na vituo vya Afya.

Jalsa salana ya mwaka huu ilifanyika kuanzi tarehe 27,28 na 29 ilikua ya kipekee kwani kaulimbiu iliyokuwa ikichagiza mkutano huu ni ISLAMU NA AMANI katika Jalsa salana mada mbalimbali zilijadiliwa na wataamu na masheikh wa jumuiya ya Ahmadiyaa pamoja na hao wageni mbalimbali wakiwemo mawaziri,wanasiasa na wakuu

UK. 03

Hotuba ya Amir Sahib Tanzania kuelekea kufunga Jalsa Salana 53 >UK .04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Shabaha ya kuumbwa kwetu

Hakuna swali lililowasumbua na linaloendelea kuwasumbua wanafalsafa na washairi kama swali, nini shabaha ya kuumbwa kwetu? kwa nini tuko hapa swali hili halikuanziwa mahali sahihi pa kulijibu. Kwanza ieleweke hatukuja huku kwa kuchagua kwetu au kwa mapenzi yetu. Aliyetuleta bila shaka ndiye anajua kwa nini ametuleta na tunawezaje kuipata ile shabaha ya kutuleta.

Aliyetuumba na kutuleta ndiye anayeelewa madhumuni ya kutuleta kwetu, katika ***The Philosophy of the teachings if Islam (Hekima ya mafundisho ya kiislamu)*** cha Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] na kutafsiriwa kwa kingereza na chaudri Sir Muhammad Zafrullah Khan[ra] katika ukurasa wa 42 shabaha tatu za maisha yetu hapa duniani zimefafanuliwa kuwa ni:-

a) Kumuelewa
b) Kumuabudu
c) Kumpenda Allah

Na shabaha hizi tatu zinaweza kupatikana kwa njia zifuatazo:-

1) Kumtambua Mwenyezi Mungu wa kweli, hatua hii ya kwanza ikikosewa basi safari yako yote itakuwa kazi bure wale wote wanaowaita kinyume na Allah hawasikii wala hawana msaada wowote. Hivyo ni lazima kumtambua Allah mmoja, hakuzaa wala hakuzaliwa Yule aliyeleta Kuruani Tukufu na kumkabidhi mbora wa viumbe wote mtukufu Mtume Muhammad[saw]

2) Kufahamu uzuri uliokamilika wa Allah siku zote moyo huvutwa na uzuri. Na Allah ndiye chanzo cha uzuri wote. Sifa zote zinazoelezwa katika kuruani Tukufu ni lazima zikuvute kwa Allah

3) Kutambua neema za Allah. Allah alimuumba binadamu na akampa mahitaji yake yote. Na kila anapofanya jambo jema anapata malipo.

4) Sala. Allah anaeleza ya kwamba-Niombe nami nitapokea maombi, mlango wa Allah uko kwa anayebisha hodi


5) Kujitolea kwa njia ya Allah kwa mali zako, vipaji vyote alivyokupa Allah na maisha yako. Vyote hivi si vyako umkabidhi Allah na utekeleze yote anayoyataka

6) Kuwa na subira, istikama. Anayetafuta asichoke. Na ahadi imetolewa kuwa wale wanaosema Allah ni Mola wetu na wakaendelea kuwa imara huteremka Malaika na huwakikishia kutokuwa na wasiwasi wowote na wafurahie bustani walizoahidiwa kwani Allah ni rafiki yao katika maisha haya na yajayo.

7) Kukaa na watu wema: kwa kukaa na watu wema unajifunza mengi na unaiga mifano mizuri kutoka kwao

8) Kupata kashf na njozi. Hizi ndio njia za kuwa na mawasiliano na Mola na njia hizi zinakuimarisha na unakuwa na elimu yakini.


Allah Atujaalie tuweze kupata shabaha ya kuumbwa kwetu.



QUR'AN TUKUFU

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

Tafsiri: «Enyi mlioamini, tafuteni msaada kwa subira na sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri.»



NUKUU YA HADITHI

قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
مَا أُعْطِيَ أَحَدٌ عَطَاءً خَيْرًا وَأَوْسَعَ مِنَ الصَّبْرِ

Amesema Mtume[saw] kuwa "Mwenye kusubiri, Mwenyezi Mungu atamjaalia. Hakuna anayeweza kupewa baraka bora na kubwa kuliko subira."



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Katika kitabu chake "Hekima ya Mafundisho ya Islam", Hazrat Mirza Ghulam Ahmad anaandika: "Subira sio kujiuzulu tu kwa bahati mbaya; ni ubora wa juu wa maadili ya uthabiti katika kukabiliana na matatizo na majaribu yote, kuweka moyo imara na kumtegemea Mungu kabisa. Ni kupitia subira ndipo mtu anapata ukaribu na Mwenyezi Mungu na maendeleo ya kiroho."- (Hekima ya Mafundisho yaUislamu)

Vyanzo hivi vinasisitiza thamani ya subira katika imani na kumtegemea Allah.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

RAIS SAMIA: AMANI NDIYO NGUZO YA MAENDELEO YA TAIFA LETU.

Kutoka uk. 01

wa mashirikia na taasisi za serikali na zisizo za serikali walihudhuria na kutoa hutuba zilizolenga katika kuimarisha jamii na kulinda haki za watu na kuwa na maadili mema. Mada tisa ambazo zilijadiliwa na watalaamu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni Mada ya 1: Jitupe kizingitini kwa Mwenyezi Mungu ufaidike na amani ya kweli hii iliwasilishwa na Sheikh Mussa Ibn Issa, Mada ya 2: Jinsi Mafundisho ya Islam yanavyodhamini Amani ya Dunia Seif Hassan Nakuchima (Katibu mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania), Mada ya 3: Uwepo wa Mwenyezi Mungu kwa nadharia ya kukubaliwa kwa Maombi katika zama za Ukhalifa wa Khalifa wa Tano (atba) Sheikh Asif Butt, Mada ya 4: Mafundisho ya Islam juu ya haki za viumbe. Sheikh Abdulrahman M. Ame - Naib Amir, Mada ya 5: Kuwasili kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Alama zake kutoka Quran na Hadithi. Sheikh Karimuddin Shams, Mada ya 6: Nidhamu ya Ukhalifa ni dhamana ya Amani duniani. (Nukta kutoka juhudi za Khalifa wa zama atba) Dr. Swalehe Kitabu Pazi, Mada ya 7: Mafundisho mazuri kwa wanandoa katika kujenga amani kwenye ngazi ya familia Sheikh Bakri Kaluta, Mada ya 8: Utii kwa Viongozi: Msingi wa kujenga amani na mshikamano katika Jamii Sheikh Ehtisham Latif, Mada ya 9: Mtume Muhammad s.a.w. - Mfalme wa Amani - Jinsi alivyowatendea maadui zake kwa wema Sheikh Abid Mahmood - Naib Amir

Kwa upande wake Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya Tanzania Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar alitoa hutuba tatu muhimu iliwemo hutuba ya ijumaa,hutuba ya ufunguzi wa Jalsa Salan pamoja na hutuba ya kufunga Jalsa Salana. Katika hutuba zote tatu alieleza kinagaubaga namna bora ya kuimarisha amani kwa kujenga mahusiano yetu na Allah kwani kama mwanaadamu atakuwa na ukaribu na Mwenyezi Mungu hii itakuwa ndio chemchemu bora ya baraka isiyokauka katika kuwahudumia viumbe Mwenyezi Mungu ikiwema kujali haki za makundi mbalimbali ya viumbe wa Allah. Akifafanua zaidi chimbuko la migogoro mingi duniani katika hutuba yake ya kufunga Jalsa Salana Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya Tanzania Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar anasema “Leo dunia imeingia kwenye dhuluma na uharibifu na nchi za magharibi hufikiria kwamba ufisadi na dhuluma hiyo ni kwa sababu ya dini na watu wanafikiria kwamba tunahitaji kwenda mbali na dini na dini imekuwa chanzo cha kuleta ujinga, uovu itikadi mbaya na msimamo mkali. Lakini uharibifu huu ni kwa sababu ya kumsahau Mwenyezi Mungu. Uharibifu huu ni kwa sababu ya kuvuka na kuvunja mipaka ya Mwenyezi Mungu na kukataa uwepo wake.

Leo dunia inashuhudia vita lakini dini si chanzo cha vita hizi. Bali chanzo cha vita ni tamaa ya nafsi na kutokufanya uadilifu. Leo upujufu umeenea katika dunia nzima lakini dini si chanzo cha upujufu huu mbali ni kwa sababu ya kuacha na kukataa amri za Mwenyezi Mungu na kuwa mbali na nuru ya Mwenyezi Mungu” Amiri Sahib alitumia nukuu mbalimbali zikiwamo Quran tukufu hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) pamoja na maandishi ya Masihi aliyeahidiwa katika kushajiisha amani katika jamii na ulimwengu. Akiendelea na maelezo yake akinukuu maandishi ya mwanzilishi wa Jumuiya Ahmadiyya Hadharat Ahamd (as) anasema; Watu wanahitaji maji ya kiroho, muda huu ardhi imekufa, zama hizi ni za ظهر الفساد فی البر والبحر yaani uharibifu umeenea katika bara na baharini msitu maana yake ni watu washirikina na bahari maana yake ni watu wa kitabu, pia maana ya bara na bahari ni watu wajinga na watu wenye elimu. Kwa hakika katika kila tabaka la watu uharibifu umeenea, dunia imegeuka kuwa mbaya mawasiliano na Mungu hayapo na athari zake hazionekani na kila mkubwa na mdogo hali ya hulka zake na vitendo vyake imedhoofika. Kwa hiyo muda huu tunahitaji maji kutoka mbinguni na nuru ya Mtume ishushwe ili mioyo ipate mwanga kutoka kwa Mwenyezi Mungu."..... Basi toeni shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwamba ametuma Masihi aliyeahidiwa (as) na sisi tumempokea lakini ni wachache wanafaidika na nuru hiyo.

Amir sahib aliendelea kusisistiza mafundisho ya uisalamu yalivyo imarisha amani kwa kutumia upendo na huruma anasema zaidi “Sisi wafuasi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tunatangaza kwa ajili ya dunia nzima kwamba islam ni dini ya amani na hakuna dini inaweza kushindana na dini ya kiislamu katika mafundisho ya amani na upendo. Dini ya kiislamu inaamuru sisi kufanya hisani zaidi ya uadilifu na baada ya hisani inaamuru kwa kuwapa watu kama uwapavyo ndugu yaani kutoa kwa ndugu bila kuendelea kumkumbusha kuhusiana na msaada uliomtolea. Kama Mwenyezi Mungu alisema: Enyi mlioamini msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia.

Sheria za dunia zimeweza kufikia hadi uadilifu tu lakini dhana ya kuwapa watu kama uwapavyo ndugu yaani kutoa kwa ndugu haiwezi kuzalika bila kufuata mafundisho ya dini tukufu ya kiislamu. Islam ndio dini pekee inayotuamuru kufanya uadilifu hisani na ujisikie uchungu na maumivu ya watu wengine ni uchungu na maumivu yako. Haya ni mapenzi bila tamaa yoyote ya kupata faida. Hivi ndivyo utaimarisha amani kwa dunia nzima”

Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya Tanzania Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar aliemdela kuukumbusha umma uliohudhuria Jalsa Salana kwa unyenyekevu mkubwa akitumia maneno laini nayakuvutia kwa kuwaita Waislamu na wasio waislamu anasema

“Ndugu zangu, dini ya kiislamu ilisisitiza sana kuimarisha na kutimiza haki za watu na hii pia ni njia mojawapo muhimu ya kustawisha amani. Kuranii tukufu ni kitabu kilichokamilika na kitabu hiki kina tiba ya kila aina ya ugonjwa wa kiroho. Hatuwezi kusuluhisha na kurekebisha na kutimiza haki za matabaka mbalimbali ya dunia kufuata Kurani tukufu. Hatuwezi kutimiza haki za binadamu mpaka tutimize haki za Mwenyezi Mungu. Masihi aliyeahidiwa (as) anasema:

"Haki za Mungu ni nini? Ni kumwabudu yeye bila kumshirikisha na yeyote nakumkumbuka yeye na kutii amri zake na kuacha yale mambo yaliyokatazwa."

Basi kama tutatanguliza Mungu lazima tutatimiza wajibu wetu aliotuamrisha, na amri zake nyingi zinahusu kutimiza haki za binadamu.Mwenyezi Mungu ana kila uwezo naye anatujalia neema za kidunia na sisi lazima tumshukuru yeye. Mtume Muhammad saw alisema mtu yeyote amefanya wema kwako basi lazima utoe shukrani kwake na bila kutoa shukrani kwa huyo mtu huwezi kumshukuru Mwenyezi Mungu kikamilifu” Mwisho wa hutuba yake akielezea uzuri wa mafundisho ya uislamu Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya Tanzania Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar alifafanua namna ambavyo haki za viumbe na haki za Mwenyezi Mungu zinavyo ungana katika kuleta amani ya kweli alieleza sifa na ubora wa Mtukufa Mtume Muhammad (saw) alivyokuwa makini mno hata katika vita alivyopigana aliweza kulinda haki hata za maiti za maadui zake na haki za mazingira. Katika nukata zake za mwisho Amir sahib alisisitiza haki mbili kubwa haki za watoto na haki za wazazi, katika haki za wazazi alinukuu Hadithi ya Mtume Mtukufu (saw) iliyosema “Hadithi: Hazrat Abdallah anasimulia kuwa nilimuuliza Mtume saw kwamba amali gani ni bora zaidi kwa Mungu akajibu kusali kwa wakati akauliza nini tena katibu kufanya wema kwa wazazi akauliza nini tena akajibu kufanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu” Amir sahib alisema kwa njia ya kuwatendea wema wazazi na kuwelea watoto katika malezi bora na kijali haki za Mwenyezi Munu na viumbe wake hiyo ndio njia bora ya kulinda amani ya kweli. Allhamdulilah Jalsa salana mwaka huu pia ilirushwa mubashara kupitia mitandao ya kijamii ikiwamo Youtube kwa siku zote tatu.

Hotuba ya Amir Sahib Tanzania kuelekea kufunga Jalsa Salana 53



إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيْتَآئِ ذِي الْقُرْبٰى وَيَنْهٰى عَنِ الْفَحْشَآءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿٩١﴾

Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamuru uadilifu, hisani na kuwapa watu kama uwapavyo ndugu na anakataza upujufu na uovu na uasi, ana wanasihini ili mpate kufahamu.

Ndugu zangu wapendwa.

Leo dunia imeingia kwenye dhuluma na uharibifu na nchi za magharibi hufikiria kwamba ufisadi na dhuluma hiyo ni kwa sababu ya dini na watu wanafikiria kwamba tunahitaji kwenda mbali na dini na dini imekuwa chanzo cha kuleta ujinga, uovu itikadi mbaya na msimamo mkali. Lakini uharibifu huu ni kwa sababu ya kusahau Mwenyezi Mungu. Uharibifu huu ni kwa sababu ya kuvuka na kuvunja mipaka ya mwezi Mungu na kukataa uwepo wake.

Leo dunia inashuhudia vita lakini dini si chanzo cha vita hizi. Bali chanzo cha vita ni tamaa ya nafsi na kutokufanya uadilifu. Leo upujufu umeenea katika dunia nzima lakini dini si chanzo cha upujufu huu mbali ni kwa sababu ya kuacha na kukataa amri za Mwenyezi Mungu na kuwa mbali na nuru ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anasema

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٤٢﴾

Uharibifu umedhihirika barani na baharini kwa sababu ya yale iliyofanya mikono ya watu ili awaonjeshe adhabu ya sehemu ya waliofanya huenda warudie. (30:42)

Mwenyezi Mungu anatuma mitume wake kwa lengo la kuondoa uharibifu ili watakaofuata nyayo zao na kujiunga nao waokolewe.

Seyyidna Ahmad (aleihi salaam) anasema:
Watu wanahitaji maji ya kiroho, muda huu ardhi imekufa, zama hizi ni za ظهر الفساد فى البر والبحر yaani uharibifu umeenea katika bara na baharini msitu maana yake ni watu washirikina na bahari maana yake ni watu wa kitabu, pia maana ya bara na bahari ni watu wajinga na watu wenye elimu. Kwa hakika katika kila tabaka la watu uharibifu umeenea, dunia imegeuka kuwa mbaya mawasiliano na Mungu hayapo na athari zake hazionekani na kila mkubwa na mdogo hali ya hulka zake na vitendo vyake imedhoofika. Kwa hiyo muda huu tunahitaji maji kutoka mbinguni na nuru ya Mtume ishushwe ili mioyo ipate mwanga kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Basi toeni shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwamba ametuma Masihi aliyeahidiwa (as) na sisi tumempokea lakini ni wachache wanafaidika na nuru hiyo.
Ndugu zangu, sasa waislamu wamepotea na wafuasi wa dini nyingine pia wamepotea, na watu wameelekea kwenye dunia na wanapenda maji machafu ya dunia lakini kwa hakika wanachofuata ni mazigazi tu. Na watu baada ya kunywa maji machafu wanakataa uwepo wa Mwenyezi Mungu na wanajiangamiza kwa kuwafuata maulamaa wabaya wanaoiharibu dini yao na pia dunia yao. Wanawapotosha pande zote mbili.

Ingawa waislamu waliitwa رحماء بينهم yaani wenye kuhurumiana wao kwa wao lakini siku hizi wanakabiliana na upungufu wa hulka njema na wanyanyima haki za watu wengine. Hii ni kwa sababu waislamu walikataa kukubali Masihi aliyeahidiwa (as) hivyo Mwenyezi Mungu akatimiza ahadi yake. Maulamaa walikataa kukubali wa zama na walipoteza watu pia wakaongoza katika upotevu, kiasi kwamba watu wa dini nyingine wakaanza kufikiria kwamba islam ni dini ya ugaidi au dini ya msimamo mkali.

Sisi wafuasi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tunatangaza kwa ajili ya dunia nzima kwamba islam ni dini ya amani na hakuna dini inaweza kushindana na dini ya kiislamu katika mafundisho ya amani na upendo. Dini ya kiislamu inaamuru sisi kufanya hisani zaidi ya uadilifu na baada ya hisani inaamuru kwa ايتاء ذى القربىٰ kuwapa watu kama uwapavyo ndugu yaani kutoa kwa ndugu bila kuendelea kumkumbusha kuhusiana na msaada uliomtolea. Kama Mwenyezi Mungu alisema:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُبْطِلُوْا صَدَقٰتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْاَذٰى

Enyi mlioamini msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia.

Sheria za dunia zimeweza kufikia hadi uadilifu tu lakini dhana ya ايتاء ذى القربىٰ haiwezi kuzalika bila kufuata mafundisho ya dini tukufu ya kiislamu. Islam ndio dini pekee inayotuamuru kufanya uadilifu hisani na ايتاء ذى القربىٰ- ujisikie uchungu na maumivu ya watu wengine ni uchungu na maumivu yako. Haya ni mapenzi bila tamaa yoyote ya kupata faida. Hivi ndivyo utaimarisha amani kwa dunia nzima.

Kwa mujibu wa dini ya kiislamu uadilifu ni wema mdogo sana ambao unapaswa kufuatwa bila shida lakini watu wa dunia wanashindwa kuzalisha khulka hii. Kurani tukufu inasema:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ لِلّٰهِ شُهَدَآءَ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلٰٓى اَلَّا تَعْدِلُوْا اِعْدِلُوْا هُوَ اَقْرَبُ لِلتَّقْوٰى

Enyi mlioamini kuweni wasimamizi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mtoao shahada kwa uadilifu, na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu huu ni karibu sana na utawa.

Katika zama ya Mtume Muhammad sallallahu alayhi wa sallam watu wawili waligombana mmoja wao alikuwa muislamu na mwingine myahudi hii ilipoletwa kwa Mtume Muhammad saw alifanya maamuzi kwamba muislamu ndiye alikosea na myahudi alishinda kesi.
Kwa bahati mbaya katika vita kuu ya pili ya dunia lilitumika bomu la atomu la mionzi mikali na watoto na wanawake ambao hawakuwa na kosa lolote waliuawa kutokana na mionzi hii. Hii ni kinyume na uadilifu badala yake Kurani tukufu inasema kuwa:

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗٓ اَسْرٰى حَتّٰى يُثْخِنَ فِي الْاَرْضِ

Haimpasi nabii kuwa na mateka mpaka apigane na kushinda katika nchi. Dini ya uislamu inakataza tusiwe na mateka mpaka vita vitokee lakini katika vita kuu ya pili ya dunia watoto akina mama na wazee waliuliwa ambao hawakushiriki katika vita.

Kisha dini ya kiislamu inasema ukiwa na mateka basi

Waacheni kwa hisani au wajipatie uhuru kwa kujikomboa. Yaani wawezeshwe kulipia ili kupata uhuru.

Kisha Mwenyezi Mungu anasema kuhusu wale mateka na watumwa:

وَالَّذِيْنَ يَبْتَغُوْنَ الْكِتٰبَ مِمَّا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوْهُمْ اِنْ عَلِمْتُمْ فِيْهِمْ خَيْرًا ۖ وَّاٰتُوْهُمْ مِّنْ مَّالِ اللّٰهِ الَّذِيْٓ اٰتٰىكُمْ

Na wale wanaotaka hati ma katika mikono yenu ya kumi basi waandikieni kama mkiwa na wema wa kwao nawapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliowapeni.

Mwenyezi Mungu alisema wale wanaotaka waachiliwe uhuru baada ya kutoa pesa basi usiwazuie lakini hatua ya pili ya hisani alisema tumieni mali yenu kwa kuwasaidia katika juhudi zao za kupata uhuru. Sasa tuangalie nani anafanya hivi? Huu ni uzuri wa dini ya kiislamu pekee ambayo ina huruma kwa binadamu na hakuna nyingine inayoweza kufika karibu na sheria hii tukufu.

Pia dini tukufu ya kiislamu imeweka sheria maalum kuhusiana na vita:
1. Katika vita adui akishauawa usiharibu uso wake wala usikate mwili wake.
2. Katika vita usiue wazee, wanawake, watoto na watu wa dini.
3. Wakati wa vita tanguliza suluhu na amani.
4. Watu wa kawaida wasioshiriki katika vita hawatakiwi kupata shida katika vita.
5. Usisababishe madhara makubwa kwa maadui wakati wa vita.
6. Mtu aliyetekwa akipewa adhabu kali pasipo haki basi fidia yake ni kwamba aachiliwe huru mara moja.
7. Watu waliotekwa wakiwa jamaa au ndugu usiwatenge au kuweka mbali bali uwaweke sehemu moja.
8. Wafungwa na mateka wapate chakula unachokipata wewe.

Ndugu zangu hii ni sheria ambayo imepita katika daraja la uadilifu na kuingia katika daraja la hisani. Hakuna mwingine siku hizi anayofanya wema kwa mateka jinsi dini ya Uislamu ilivyofundisha. Hii ni njia moja wapo ya kuzima moto ya vita na si kufanya vita.


Ndugu zangu waislamu walipata maendeleo ya hali ya juu sana waliposimamia uadilifu na hisani. Lakini walipoacha hulka hizi maendeleo yao yakakatika. Hivyo tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kusimamia uadilifu, tufanye hisani na tuzingatie ايتاء ذى القربىٰ kati yetu ili amani, mapenzi na huruma zistawi duniani. Aamin

Ndugu zangu, dini ya kiislamu ilisisitiza sana kuimarisha na kutimiza haki za watu na hii pia ni njia mojawapo muhimu ya kustawisha amani.

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

MUHAJIRINA KATUTOKA

Na; Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Kiwalani Dar es Salaam



1952 - Katika kijiji cha Mtandi-Kilwa (Kilwa ni neno la kiarabu 'Kill a' maana yake ngome madhubuti) marafiki watatu wenye hofu ya Allah pekee walichukua uamuzi wa hekima wa kumpokea Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] na hivyo kujiunga na jumuiya ya Ahmadiyya.

Marafiki hao ambao historia ya Ahmadiyya nchini Tanzania na nje ya mipaka yake huendelea kuwakumbuka na kuwaenzi ni Sheikh Issa Harun Kurunguja, Mohamed Selemani Mkoka Sahib na Abdallah Mshamu Dungurusi Sahib. Hawa ndio muhajirina wa kwanza nchini Tanzania ambao waliacha palipo vitovu vyao si kwa sababu yoyote ile bali kutimiza maagizo ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw] aliyesema Masih akidhihiri hata kama ni kutembea kwenye theluji kumfikia fanya hivyo. Na kweli kujiunga na Ahmadiyya katika miaka ya 50 ilikuwa mithili ya kutembea juu ya theluji.

Marafiki hao watatu baada ya kupata ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa (as) walipambana na dhuluma na mikasa ya kila aina. Hakuna kupokea Assalam Alaykum yao, wasizikwe, kilele cha mateso lilikuwa jaribio la kuwanyang'ang'anya wake zao. Akina mama hao shujaa wakionesha ushujaa ulioneshwa na akina mama wakati wa vita vya uhud walisimama kidete kutetea haki yao ya kuabudu. Hakuna aliyemuacha Mume wake. Mateso yaliendelea na kuzidi na hivyo sheikh Fadhilillah Bashir, Sheikh … Ahmad Mataka Busra, mzee Karuma Issa wakawashauri wanajamaat hao imara kuhama kutoka Mtandi kuja Mtama Lindi, hali ya Kilimo haikuwa nzuri na Sheikh Abdulkarim Sharma akawashauri kuhamia katika ardhi yenye rutuba Rufiji. Walifanya hivyo na katika kuhama walikuwa na watoto ambao umri ulikuwa mdogo lakini baadae wakawa wanajamati wenye msimamo thabit na kuitumikia Jamati. Hao ni Mwalim Othman Mkoka na Fadhil Abdallah Mshamu Dungurusi ambaye tarehe 23/08/2024 aliitikia wito wa Mola wake na kuzikwa katika makaburi ya Jamati na umati wa watu siku ya jumamosi tarehe 24/042024 sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Fadhil anaungana na wale



waliopewa majina ya mashehe waliofanya kazi kubwa ya kueneza mafundisho sahihi ya Islam, hao ni inayatullah, Jamil na Munawar yeye alipewa jina la Fadhillah mbashiri ambaye aliyoyafanya huko kusini vigumu kusahaulika.

Nilifahamiana na Fadhil Mshamu Dungurusi Sahib toka 1965 nilipokuwa shuleni na nikiishi msikitini. Wakati huo alikuwa Goba. Nakumbuka adha za usafiri za siku hizo lakini alikuwa anakuwa wa kwanza siku ya Ijumaa akikaa msitari wa mbele akifanya dhikri. Tabia ya kufika msikitini na kuanza porojo zisizokuwa na uhusiano na msikiti hakuwa nazo. Hulka yake ya upole iliwavutia wengi na akawa amejijengea urafiki wa karibu na wanajamaat wengi. Swala la sala alilipa kipaumbele na popote alipo alitafuta msikiti wa jamati na hata kama ilikuwa na maana ya kutembea maili nyingi kuufikia msikiti ulipo. Taarifa tulizozipata kutoka kwa watu wake wa karibu ni kwamba hakughafilika hata kidogo kuhusu sala ya Tahajud. Aliitekeleza na kuwahimiza akhli zake na wajenge utamaduni huo.

Ibada inamuweka mbali mtu kufanya mambo yasiyokubalika, Fadhili sawa na jina lake aliwafadhili ndugu na jamaa kwa mapenzi na huruma. Ukimsikia mtu amegomba na Fadhili Sahib lazima apelekwe hospitali bila shaka atakuwa na kasoro fulani. Hakupenda ugomvi wala shari na mtu yeyote. Majirani zake waliona raha kuwa karibu naye akikumbuka Hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ya kuwatendea wema majirani.

Ukimkuta Fadhili Sahib kainamisha kichwa basi uelewe fikra zake ziko kwenye michango. Kama hajatoa michango roho yake haitulii, sio kutotoa bali kuchelewa tu kulimpa wasiwasi. Lakini kwa ujumla alikuwa mtoaji mzuri wa michango kwa wakati, anafariki tayari alikwisha toa mchango wake wa mwezi wa saba na katibu wa Taifa wa Wasiyya Mohamed Ussi Sahib anasema wiki mbili kabla ya kifo chake alimpigia simu na kumuuliza kama mambo yake yako sawasawa. Katibu wa wassiyat anaeleza kuwa Fadhil Sahib alikuwa tayari amekwisha lipa Hisa Jaidad kwa ukamilifu sambamba na kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za Jamati. Alikuwa ni Raisi wa Tawi la Kitanga-Katika wadhifu wake huo alihudhuria mikutano yote na kuja na taarifa za tawi lake zilizokamilika.

Miaka ya baadae uhusiano wetu ulizidi nilipogundua kuwa alikuwa na mambo mengi ya muhimu kuhusu historia yetu, mengi alikuwa nayo kutokana na sababu mbili. Yeye ni mtoto wa mzee mshamu ambaye yeye pamoja na Sheikh Isa Kurunguja na Mohamedi Mkoka walipata heshima ya kuwa Muhajirina wa kwanza kuondoka mahali walipozaliwa kutokana na uhasama dhidi ya jumuiya ya Ahmadiyya na sababu ya pili mke wake bi Zainabu Mbungiro ni binti wa Mshairi maarufu wa kiswahili Malik Abdallah Mbungiro Sahib ambaye kalamu yake iliwatangazia maadui wa Jamati kuwa watachoka, kwa sababu hizi mbili kila nafasi ilipopatikana alinisimulia mateso waliyoyapata na juu ya Baba mkwe wake watachoka. Bila ya yeye sehemu muhimu ya historia yetu si ajabu ingeishia kwenye kaburi la sahau. Jambo lililonifurahisha juu ya Fadhili Mshamu Sahib ni kwamba wakati wote alikuwa tayari kunipa maelezo na majibu ya maswali wakati naendelea kuandika historia ya Ahmadiyya Tanzania katika hili alikwenda maili moja zaidi na akaandika makala kuhusu kuhama kwao, makala ambayo imechapishwa katika Mapenzi ya Mungu. Licha ya kuwa mwandishi mzuri alipenda sana kusoma. Allah Amlipe yaliyo mema na sisi tuliobaki tuna mengi ya kujifunza kutoka kwake.

Bustani ya Washairi

MUHAJIRINA

Kwa jina lake Kahari
Alomtuma bashiri
Leo ninayo habari
Imenigusa moyoni

Japo ninao uchungu
Hayo mapenzi ya Mungu
Atakalo toka enzi
Linabidi duniani

Lina budi kutokea
Alipendalo Jalia
Mwumbaji wa dunia
Kwake kun fayakuni

Habari ni za msiba
Kafariki wetu baba
Alokuwa na mahaba
Wote walio kundini

Yeye na wake wazazi
Safari ile Azizi
Walikuwa viongozi
Mtandi hadi Jangwani

Mpenzi mambo ya kale
Hijira ile teule
Nyuma ameacha shule
Kahifadhi gazetini

Kaeleza kwa undani
Kuwahusu wapinzani
Walishindwa mtihani
Wakazama mashakani

Tutakumbuka daima
Na tena kwa taadhima
Kazi ile ya lazima
Itakuwa vitabuni

Alishika sana dini
Fadhili mtu makini
Hakuacha asilani
Kufika msikitini

Na sala ya Tahajudi
Kwake ilikuwa budi
Kaifanya yake Jadi
Kwa machozi kifuani

Michango hakuwa nyuma
Alitoa hima hima
Hadi ya kupata homa
Kama hana mfukoni

Alidumu kwa hisani
Kwa ndugu na majirani
Bughudha abadani
Hakuwaudhi insani

Mikutano ya Jamati
Alifika kwa wakati
Kushiriki harakati
Ili vikao viwini

Fadhili bin Mshamu
Tunaomba kwa karimu
Apate pepo adumu
Kwa jala yake manani

Azipokee wadudi
Zile za kwake juhudi
Za kupigania jihadi
Utakaso wa moyoni

Kaditamati wa tama
Kwako Mola twasimama
Twamuombea rehema
Yakuwepo kivulini.

Mahmoud Hamsin Mubiru(wa mamba)
Kiwalani-Migombani

YAKINI

Kikombe kimetakata, kwa nje kinavutia
Kwa kila anayepita, mate anakimezea
"Na mimi ningekipata, fuadi ingetulia
"kumbe siri ya maiti, aijuae muosha!

Pamwe na mshika kata, maji anayemwagia
Kimya huwa aina sita, lolote kujisemea
Kila mpenda kubwata, kichwani zimepungua
Akatula omungoma, kamanywa omubambi

Uzuri wenye kumeta, ni ndani kuchungulia
Yaliyomo ni mafuta, au uchafu ajaa
Bila yakini tajuta, katika hino dunia
Tizama nje na ndani, kuupata utulivu

Kaditama hujapata, bileshi wajisumbua
Yakubidi kujikita, kiini kukifikia
Au utaula mwata, janga utajivunia
Na kila mvuna janga, hula pamoja na wake

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

WAPOKEAO NABII

Mola Aliye Shafii, nitukuze lake jina.
Mbele yake nijidhii, nimhimidie sana.
Nimsalie nabii, Bwana wa murisalina.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Nauliza maqarii, wenye ujuzi mpana.
Wajibu nukuta hii, kwa maelezo mwanana.
Kwa hoja zilo rafii, isiwe kwa kutukana.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Katika dunia hii, kuna mengi yaso mana.
Na wanaoyatabii, hujidhani waungwana.
Wakajipa uwalii, na vyeo vya abidina.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Kiasi nimetalii, Kuruani ya Rabana.
Kwa yangu kubwa bidii, ndani mwake sijaona.
Walomtii nabii, kuitwa waja laana.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Masahaba, matabii, na tabii tabiina.
Hawa wote walitii, miito ya nabiyina.
Lakini hatusikii, wakiitwa kafiruna.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Walopinga manabii, kwa kiburi kuwakana.
Rabi amewanazii, kitabuni kawanena.
Akawafifiza fii, heshima akawapuna.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Hawa wafanya bidii, leo tuaowaona.
Wakipinga unabii, wakiupaka laana.
Watujuze dhana hii, wapi walikoivuna.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Wasihoji kisanii, kwa hoja walizosana.
Bali dalili katwii, watuwekee bayana.
Wallahi hatubishii, kweli tukishaiona.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Kama kwa nyoyo za sii, na chuki ilowabana.
Ndipo wakazira zii, watumwao kuwakana.
Punde Watatimbwa tii, kwa timbo la Subuhana.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Nawapa nasaha hii, wenye macho ya kuona.
Kwamba huu unabii, ni neema ya Rabana.
Waja wanapoutii, baraka hupatikana.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Keshatangaza Wasii, Muumbaji Maulana.
Kwamba kupinga nabii, ni kufuru kubwa sana.
Iwapo hawasikii, mwishowe watayona.
Vipi wapewe laana, wapokeao nabii?

Al Ustadh, Abu Talha, Abdullah H. Mbanga
(KUNGWI)

Jana na leo

Ee mola wangu muweza, uzuri ulojaliwa
Niepushe Kwa uweza, ubaya kuniondowa
Uzuri wako nijaza, sifa zako elezewa
Nisafishe mola wangu, tope za Jana na leo

By
Masihi Omary Stambuli Kisagwa

DUNIA SIIDEKEZE

Mola mwenye Kuhuluku, isimuye nitanguze.
Nimuombe kwa shauku, udata anifunguze.
Nisitongoe ushaku, na manju wanipuuze.
Dunia siendekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia ni chakubimbi, hazina nyemi sikuze.
Ninamaka kwa ulumbi, zingatia usibeze.
Hili si neno la hambi, ni ndefu sana zamaze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia siyo yambone, ni lukuki hadaaze,
Fanya juhudi upone, usisombwe na rahaze.
kiifanya mti pane, tajuta kwa ikabuze.
Dunia siendekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia rangi rangile, si za ukweli rangize.
Siifate kwa jefule, hima usiikimbize.
Takufanya kitundule, na thamani ikuvize.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia ina hadaa, hadharani nitangaze.
Usiridhi kuduwaa, kwa kuokota tondwaze.
Mwishowe utabug'aa, muda wako upoteze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia ni narabuku, si hasha ikuduwaze.
Uyendeapo mkuku, kufakamia shanize.
Utabaki matuluku, Rabi akutelekeze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia ni kama tanzi, lilo na ngumu fundoze.
Itakupa makunyanzi, moyoni ikuzeveze.
Kamwe usiipe penzi, jihadhari na tunuze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Dunia ni mazigazi, na zinaghuri njiaze.
Itaja kupa uchizi, ukitabii konaze.
Ina vingi viumbizi, kwa utamu wa sumuze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Kungwi nakomea hapa, utungo niukatize
Huku roho yanipapa, kutaka wanisikize.
Waendeao kwa pupa, dunia na fanakaze.
Dunia siidekeze, siyo rafiki kinaya.

Abu Talha, Abdullah Hamisi Mbanga(Kungwi)
Radio Ahmadiyya 99.3 Mtwara.

BADO UNANIKUMBUKA?

Bado unanikumbuka, Bado unaniombea
kazi nilishughulika, Kupambania familia
Pamoja kuimarika, Malengo yalitimia?

Wewe hukujali hali, Mali wala madaraka
Na ulikuwa kivuli, Kwangu vyote hujengeka
Bado unanikumbuka, Bado unaniombea?

Nilipenda kujituma, Tumaini na maombi
Riziki tukazichuma, Tukaota na vitambi
Tukazitunza amana, Bado unanikumbuka?

Ukazichagua nyemi, Sio mpambanaji
Nami nikawa mtemi, Na ukatumeza mji
Msongo hautuhami, Bado unaniombea?

Nilikuwa kweli mume, Nawe mke bora sana
Kipindi hakuna meme, Haki tulipopeana
Bado unanikumbuka, Bado unaniombea?

Kupatana ni muhali, Bila kubadili hali
Tusahihishe amali, Kwa Mungu pawe mahali
Bado unanikumbuka, Bado unaniombea ?

Hadithi ya Hamasa ya Kiislamu:

Jifunze kutokana na Makosa

Thomas Edison alijaribu vifaa elfu mbili tofauti katika kutafuta filamenti ya balbu ya mwanga. Wakati hakuna aliyefanya kazi kwa kuridhisha, msaidizi wake alilalamika, "Kazi yetu yote ni bure. Hatujajifunza chochote."



Thomas Edison alijibu kwa kujiamini sana, «***Oh, tumetoka mbali na tumejifunza mengi. Sasa kuna vipengele elfu mbili ambavyo hatuwezi kutumia kutengeneza balbu nzuri ya mwanga.***"

Nukuu ya Kuhamasisha: "Ikiwa utajifunza kutokana na makosa yako basi una akili. Lakini ukijifunza kutokana na makosa ya mtu, basi wewe ni Mjuzi."

Nukuu ya Kutia Msukumo: Mafanikio si chochote zaidi ya taaluma chache rahisi zinazofanywa kila siku na kutofaulu si chochote zaidi ya makosa madogo machache yanayorudiwa kila siku.


Jinsi ya kweli, mistari hapo juu ni! Mafanikio au kushindwa hukita mizizi katika akili zetu. Wakati hatufanyi nidhamu maishani, hatujengi ujasiri wa kutosha kujaribu kazi mpya na zenye changamoto ambazo ni muhimu na muhimu maishani. Kujiamini kwetu kunategemea kile tunachojifikiria sisi wenyewe na ikiwa tunajiamini wenyewe. Sote tumezaliwa na sifa za kipekee lakini ni wachache tu wanaotambua uwezo wao wa kweli na kusonga mbele maishani na wengine wanaishi maisha ya wastani. Je, ungependa kufanya ya kipekee?

Mafanikio ni tunda ambalo kila mtu anatamani kula lakini halipatikani kila mahali na hakuna anayeweza kuyapata bila juhudi za dhati.

Wale wanaotaka kufanikiwa watapata njia, wale ambao hawatapata watapata kisingizio!
Mafanikio yanategemea maandalizi ya awali, na bila maandalizi hayo kuna hakika kuwa kushindwa.

Unapofanikiwa watu wanaokutakia mema wanajua wewe ni nani? Unapokosa mafanikio unajua wanaokutakia mema ni akina nani?

Unganisha Nukta kupata Mchoro



SHIRIKA LA HUMANITY FIRST LAHIMIZA JAMII KUCHANGIA DAMU









Shirika la humanity first kwa kushirikiana na Taasisi ya Jamia Ahmadiyya Tanzania waliendesha kampeni maalum ya kuhamasisha jamii kutambua na kuona umuhimu wa kuchangia damu salama kwa ajili ya kuokoa maisha ya watoto, kinamama wajawazito na watu mbalimbali wenye uhitaji. Kiongozi wa shirika la Humanity first hapa nchini Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib ambaye pia ni Principal (mkuu wa chuo) Jamia Ahamadiyya Tanzania ndiye mratibu wa shughuli hii. Uzinduzi wa zoezi hili ulifanyyika sikuya jumatano tarehe 11/September 2024 katika eneo la soko kuu la Mkoa wa Morogoro-Maarufu Chifu kingaru.

Mgeni rasmi katika uzinduzi wa shughuli hii alikuwa ni Mheshimiwa Sahibzada waleed ahmad sahib Naib mkurugenzi mkuu wa shirika la Humanity first Marekani.

Jumla ya Unit 29 zilipatikana ambapo makadirio yalikuwa ni kupata unit 25 Al-hamdulillah. Akielezea shabaha ya zoezi hilo, kiongozi wa shirika la Humanity first hapa nchini Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib alisema "lengo la taasisi hii ni kujaribu na kufanya kila aina ya jitihada ili kupunguza na ikiwezekana kuondolea mbali changamoto zinazowakabili wanadamu".

Hivyo alitoa wito kwa jamii kuunga mkono juhudi zinazofanywa na shirika hili ili kufikia malengo na kuiletea faraja jamii yenye uhitaji. Habari za tukio hili zimetangazwa katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii na gazeti la **Habarileo,** toleo na.00356 la jumanne tarehe 17/09 /2024.

Ujumbe wa Huzur[atba] katika Jalsa Salana Tanzania 53

...Kutoka uk.12

'Haya ni mambo na masharti ambayo nimekuwa nikiyahimiza tangu mwanzo, na ni wajibu kwa kila mwanajamaat wa Jumuiya yangu kuyafanyia kazi. Hampaswi kujiingiza katika uchafu, kebehi au dhihaka. Tembeeni juu ya ardhi kwa mioyo iliyo mizuri, dhana njema, na mawazo safi. Sio kila uovu unafaa kupigana nao, kwa hiyo jengeni tabia ya kusamehe na kupuuza madhaifu ya wengine na ishini kwa uthabiti na unyenyekevu. Msimshambulie mtu yeyote visivyofaa na wekeni matamanio yenu chini ya udhibiti kamili. Ikiwa mnashiriki katika majadiliano, au katika kubadilishana mawazo juu ya somo la kidini, jieleze kwa upole na kuwa na adabu. Mtu akikukoseeni, basi ondokeni katika kundi hilo kwa salamu ya amani..... Mwenyezi Mungu anataka muwe Jamaat yenye kuwa kielelezo cha wema na ukweli kwa ulimwengu wote.'

(lshtihar (The Announcement), May 29, 1898. Majmu'ah lshtiharat, vol. 3, p 46)

Ninakusihini daima muishikilie taasisi ya Kimbingu ya Khilafat-e-Ahmadiyya. Mnapaswa kujitahidi kutengeneza mafungamano ya karibu na Khalifatul Masihi na kubaki waaminifu milele. Mnapaswa pia kuwafundisha watoto wenu neema zisizo na kipimo za Ukhalifa na kuhakikisha kwamba vizazi vyenu vijavyo vinaendelea kubaki ndani ya mwongozo uliobarikiwa, ulinzi na mwamvuli wa Ukhalifat-e-Ahmadiyya. Mnapaswa kutazama MTA mara kwa mara na kuzihimiza familia zenu, hasa watoto wenu, kufanya hivyo pia.

Ninamkumbusha kila mwanachama wa Jumuiya juu ya umuhimu wa kuhubiri. Katika hotuba yangu ya Ijumaa ya tarehe 8 Septemba 2017, nilisema:

Kama sisi tutaulizwa, itakuwa kiasi hiki, ambacho Mwenyezi Mungu Aliyetukuka atatuuliza, Je tumefikisha ujumbe? Au kwa nini hatujatimiza wajibu wetu wa kufanya Tabligh? Au kwa nini hatujatekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka? Kuendelea kufanya kazi mfululizo ni kazi yetu, kazi yetu ni kuhubiri, kufikisha ujumbe. Kuwapatia watu mafundisho mazuri ya Uislamu ni kazi yetu na lazima tuendelee kufanya hivyo.

Kwa hivyo, mnapaswa kupanga kwa busara na kutafuta njia mpya za kueneza ujumbe wa amani wa Islamu Ahmadiyyat kwa watu wote wa Tanzania.

Kwa kumalizia, ninawaambia ninyi nyote - kwamba sasa ni wakati wa kujitokeza na kuahidi kwa azimio kamili na thabiti kwamba mtatafuta milele kuleta mabadiliko yote safi maishani mwenu ili muweze kutii na kutimiza kila moja ya masharti ya Bai'at tuliyoahidi kwa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Isha'Allah. Kama ninyi mtafanya hivyo, basi mtaweza kuleta mapinduzi ya kweli ya kiroho duniani.

Mwenyezi Mungu akuwezesheni kuufuata mwongozo huu kwa njia iliyo bora zaidi.

Mwenyezi Mungu akubariki nyote.

Wassalaam

Wenu Mwaminifu


Imesainiwa na

MIRZA MASROOR AHMAD


KHALIFATUL MASIH V

MATUKIO KATIKA PICHA



















Mwana Mkuu wa Ibrahim

Siku chache zilizopita nimewahi kuona makala moja ya mwalimu wangu ***Maulana Jamil ur Rahman Rafiq*** aliyoiandika kwa gazete la Al-fazl International. Baada ya kuisoma na kusisimka nimeonelea vyema kuandaa muhtasari wake kwa ajili ya ndugu zangu wasomaji wa 'Mapenzi ya Mungu'. Mwana Mkuu Wa Ibrahim aliandika ***Maulana Sheikh Jamil ur Rahman Rafiq*** mnamo 1977 ili kuhakikisha ubatilifu wa madai yaliyofanywa katika kitabu cha 'Wana wa Ibrahimu' kilichoandikwa na ***Padre H.P. Anglars***, ambacho kilichapishwa Tabora na kilikuwa na kurasa 200. Padre alijaribu kueleza humo kwamba Wakristo na Waislamu wote ni wana wa Ibrahimu, lakini bahati mbaya Waislamu wamepotea njia, na dhamira yake ya kuandika kitabu 'Wana wa Ibrahimu' ni kuwafanya Waislamu kuwa wana wakweli wa Ibrahimu. Kidhahiri Padre alitumia maneno matamu ili kuwavutia, lakini kwa hakika aliuma na kupuliza. Akaleta upinzani mkubwa dhidi ya Mtume Mtukufu[saw] na dini ya Kiislamu, kwa mfano kuhusu utumwa, mitala, vita vya Mtume[saw] , shungi, na kuoa mke wa mwana wa kupanga aliyetalikiwa. Kitabu hicho kililetwa Dar es Salaam pia na kuuzwa katika duka la mauzo ya vitabu vya Kanisa la Katoliki.

Hasira zikaibuka kati ya Waislamu, lakini hawakuweza kujibia tuhuma hizo kwa namna yoyote ile. Suala hili lilijadiliwa katika Majlise Shura ya Tanzania mwaka huo, na yakafanywa maamuzi ya kutoa majibu yake. Miaka hiyo hali ya Jamaat kifedha haikuwa nzuri sana, hivyo ikaamuliwa kuchapisha majibu hayo kidogo kidogo kila mwezi ndani ya ***Mapenzi ya Mungu***.

Maulana amesimulia tukio moja katika makala yake kuwa siku moja nilipokuwa nafanya kazi ya Jamaat ofisini kwangu, walinitembelea ndugu wawili, mmoja wao alikuwa mwanajumuiya Bw. Abu Bakr na mwingine alikuwa Bw. Muhammad Salim Kungulilo — ambaye moyoni alishakubali Uahmadiyya kwani alikuwa anatoa michango sawa na kiwango, alikuwa anaupenda ukhalifa, lakini alikuwa anasita kujaza fomu ya baiati. Kila siku akasali Magharibi na Isha msikitini mwetu, na zingine alikuwa anasali nyumbani kwake. Ndugu huyo alikuwa anahubiriwa na Maulana Muhammad Munawar aliyekuwa
Amiri na Mbashiri wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania kabla yangu. Sheikh Jamil anasema:

Nilipopewa jukumu la uamiri nilimhimiza kujaza fomu ya baiati jambo lililo muhimu sana, kwani alikuwa Muahmadiyya kimoyo na kivitendo. Lakini Bw. Muhammad Salim Kungulilo
alikuwa na wazo kwamba kujaza fomu ya baiati na kuitia saini siyo lazima sana.
Aliposisitizwa aliniambia kama nitafanya baiati basi nitafanya kwa mkono mtukufu wa
Hadhrat Khalifa tul Masihi III huko Rabwah. Maulana anasema: Nilikuwa namwita asiye mwanajumuiya ili kumhamasisha kufanya baiati, lakini wapi bwana Muhammad Salim Kungulilo alikuwa anang'ang'ania kutofanya baiati kwa kusema mimi ni mwanajumuiya.

Walipowasili hao wawili ofisini wakaniambia kwamba tunataka utuahidi jambo moja, lakini jambo lenyewe hatutokuambia hadi ufanye ahadi nasi kwamba lazima utalikubali.

Maulana anasema: Nikawaambia sharti mnaloweka haliko la Kiislamu, kwani wakati mimi sijui mnanitaka nifanye jambo gani, nawezaje kuahidi kulitekeleza? Kwa mfano kutekeleza ahadi kungekuwa nje ya uwezo wangu hapo nitafanyaje? Wote wakasema uwezo unao.

Nikawaambia sawa kwa mtazamo wenu uwezo ninao, lakini yawezekana kihalisia sina uwezo. Nikasema kwa vyovyote vile basi mniambieni kisha nitafanya maamuzi.

Wakasema tunataka uandike jibu la kitabu cha Padre Anglars kwa sura ya kitabu. Kwa kulisikia hili nikamwambia Bw. Abu Bakr kuwa huyu si Muahmadiyya, lakini wewe ni mwanajumuiya na unajua vyema kwamba mwaka huu katika Shura yetu tumekubaliana kutoa majibu yake kidogo kidogo ndani ya gazeti letu la ***Mapenzi ya Mungu*** kwani Jamaat kwa sasa haiwezi kubeba gharama ya uchapishaji wa kitabu kizima. Bw. Kungulilo mara moja akasema nami pia ni mwanajamaat. Basi wote wawili wakaniambia tumekujia na suluhisho la suala hili hili kuwa tutabeba nusu nusu gharama ya uchapishaji wa kitabu hicho.
Nikasema sawa, nitamwambia mwandishi mzuri Muahmadiyya kuandaa jibu lake.

Wakasema, hapana tunataka uandike majibu wewe. Basi, nikawaahidi kuandika majibu.
Baada ya kufunga ahadi ya kuandika kitabu nikamwambia Bw. Kungulilo, nimekubali ombi lako lakini ukubali ombi langu, Bw. Abu Bakr alishindwa kuelewa nilichosema. Bw. Kungulilo alisema nimekubali na akaniomba fomu ya baiati, aliyoijaza na kusaini na akawa Muahmadiyya rasmi. Baadaye alienda London kushiriki mkutano wa Kasre Salib
(Kongamano la Uvunjaji wa Msalaba). Alhamdu-Lillah. Alipoonana na Khalifa Mtukufu III aliweza kupiga picha pamoja naye na baada ya kurudi nyumbani aliongeza ukubwa wa picha hiyo na kutia ukutani nyumbani mwake ambayo picha hiyo alikuwa anajivunia sana.

Maulana Jamil ur Rahman anasema: Nikatia bidii sana na baada ya kushugulikia kazi hii usiku na mchana katika muda si mrefu nikaweza kuandika jibu la kitabu hicho cha Padre.

Wakati wa kujibu shutuma za Padre nilipanga kitabu changu kwa mpangilio huu kwamba nilipanga milango sawa na milango ya kitabu cha Padre, hata kila mlango ukapewa kichwa cha maneno sawa na kichwa cha maneno cha mlango wa kitabu cha padre. Na majibu yaliandaliwa sawa na hoja za mantiki zilizotumika na ***'jicho kwa jicho'*** za Sayidina Ahmad as .
Alipojaribu Padre kudhihaki akajibiwa kwa namna ya kumkosesha utovu.

Kujibu kwamba Waislamu wamepotea njia iliyo sawa, akaambiwa, wana hasa na wakweli wa Hadhrat Ibrahimu as ni wale tu wanaofuata nyayo zake. Hadhrat Ibrahimu as alitii agizo la Mungu la Tohara na alianzisha sheria ya kutahiriwa. Waislamu wanafuata agizo hili kwa msistizo mkubwa.

Lakini Wakristo waliipuuza sheria hii kusudi na kulifutilia mbali agizo hili la Nabii Ibrahimu[as]. Basi, hebu tuone nani hasa ni wana wa Ibrahimu na nani amekwenda kambo?

Halafu, Hadhrat Ibrahimu[as] aliendelea maisha mazima kuhubiri Umoja wa Mwenyezi Mungu – jambo ambalo kwa sababu yake kaumu yake walitaka kumchoma moto. Lakini Mungu Mwenye enzi Alimlinda.

Waislamu wanashikamana na Umoja wa Mwenyezi Mungu, Islam inafundisha لَمْ يَلِدْ وَ لَمْ يُوْلَدْ. Lakini Wakristo wameasi agizo la tauhidi na wamebuni miungu watatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hivyo, Waislamu ndio wana wakweli wa Nabii Ibrahimu, na Wakristo ndio waliopotea njia.

Kuhusu utumwa, Padre aliandika kwamba biashara ya watumwa ilikuwa imezoeleka sana Uarabuni hata kabla ya Uislamu, ndiyo maana Biblia inataja kuwa waliomnunua Hadhrat Yusufu[as] kama mtumwa ulikuwa msafara mmoja wa wana wa Ismail. Akajibiwa: Bw. Padre, umekumbuka vizuri kwamba waliomnunua Nabii Yusufu[as] kama mtumwa walikuwa wana wa Ismaili, lakini umesahau kuwa waliomwuza mtumwa huyo walikuwa wana wa Isreal?

Padre alijasiri na kuandika zaidi juu ya suala hili kuwa Waarabu walitunza vyema desturi hii ya mababu zao na waliendelea kufanya kazi ya kununua watumwa kutoka bara la Afrika. Akajibiwa kama walifanya hivyo walienda kinyume na mafundisho ya Islam. Tena, ujue vizuri waliofanya hivyo hawakuwa wataalamu wa dini, walikuwa wafanya bishara tu; lakini mapadre wa Katoliki kwa idhini ya Papa Leo II walinunua

Ukurasa wa 11

Mwana Mkuu wa Ibrahim

Kutoka 10..

watumwa wengi kutoka Afrika, halafu meli mbili walizotumia mapadre ili kuwachukua watumwa hao, moja yao iliitwa jina Jesus (Yesu) na nyingine Mary (Mariam). Hivyo wasomaji wenyewe wanaweza kulinganisha pande zote mbili, na kuona tofauti. Almuradi majibu ya shutuma zote yaliandaliwa sawa na mtindo wa Sayidina Ahmad[as] kujibu upinzani kama huu, ambao hatuoni haja kutaja tena.

Nikamaliza kuandaa majibu ambayo yalienea katika kurasa zaidi ya mia mbili. Nikayapitia tena na kuridhika kwamba majibu yanatosha kumnyamazisha kila mpinzani mwenye chuki ya bure. Alhamdu Lillah na nikamshukuru Mungu. Mwishoni nikafasiri beti kadha na nudhumu moja ya Sayidina Ahmad[as], kwa sura ya nudhumu za kiswahili; k.v.

Muhammadi muongozi, ndiye wetu kiongozi, aloleta nuru hizi, yu mpenzi wangu miye.
(beti chache)
Sisi tu shujaa watu, sojali bughudha katu,
nyoyo zetu madhubutu, uchungu twavumilia.
(beti chache)
Nisikieni jamani, hawaipati auni, mlangoni pa Manani, rohoni walochafuka.
(shairi zima)

Mashairi yanapendwa sana Tanzania, na wapo washairi wengi mabingwa nchini. Nami naona Waahmadiyya wamefurahia sana beti hizi chache na fuadi zao zitasisimka. Basi kitabu kilimalizika. Ningependa kutaja baadhi ya matukio kadha yaliyotokea siku hizo.

Siku moja Muahmadiyya mmoja aliyekuwa maneja wa benki fulani akaja kwangu na kunisimulia kwamba mapadre wazungu waliokuwa wanaagiza mitumba ya nguo zilizotumika kutoka Ulaya mmojawapo alikuja benki leo kuchukua mtumba wao. Hakujua kuwa mimi ni mwanajamaat. Wakati wa kuzugumza nami akasema: Waahamdiyya wameandika kitabu dhidi yetu, tulimwendea Rais ili kitabu chao kipigwe marufuku na kizuiliwe. Rais kwa kukiona kutoka kwao kitabu hicho alisema haina haja kukipiga marufuku, bali kinachohitajika ni kuandaa jawabu lake tu.

Maulana anasema wakati kitabu kilikuwa hakijapelekwa mtamboni kwa ajili ya uchapishaji, nilitafakari sana nikipe jina gani? Na nilipenda kuwa kama kila mlango wa kitabu hiki umeushinda kila mlango wa kitabu cha Padre, jina lake pia lishinde jina la kitabu chake.

Niliwaza sana kuhusu jina lakini sikuweza kupata jina lishindalo jina la kitabu cha Padre Anglars. Padre alishatumia jina ‘wana’, hivyo mbali na ‘wana’ wanaobakia ni ‘wajukuu’ au ‘vitukuu’ na ‘watukuu’. Anasema nilishauriana na baadhi ya Waahmadiyya wasomi wa Dar es Salaam ambao miongoni mwao mmoja alikuwa mzee Rashidi Msabah Rais wa Jumuiya ya Dar es Salaam. Wote walitaamali sana lakini hawakuweza kupata jina lishindalo jina la kitabu cha Padre. Basi, sikuwa na chaguo jingine ila kukipa jina ‘Wajukuu wa Ibrahimu’ shingo upande na kupeleka matbaa.

Siku zikapita nyingi hadi nikasahau suala la jina la kitabu hiki. Usiku mmoja nilipoamka kwa ajili ya swala ya nafali, ghafula nikatiliwa kwa nguvu rohoni (إلقاء) Mwana Mkuu Wa Ibrahim. Nikashtuka, nini hii! Haraka nikafahamu, hili ndilo jina la kitabu changu.

Nikamshukuru Mola Karimu. Mwana Mkuu maana yake ni Mwana Adhimu na Ajwadi. Jina hili kweli lilikuwa linalishinda jina la kitabu cha Padre. Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe amesema اَنَا دَعْوَةُ اَبِیْ اِبْرَاهِیْمَ kwamba mimi ni tunda la maombi ya baba yangu Ibrahimu.

Alhamdu Lillahi. Nikafurahi sana na nikamshukuru Mungu. Basi asubuhi nikaenda maktaba kuuliza kitabu kimefika hatua gani? Wakaniambia twaendelea kuandika kwa kampyuta.
Nikauliza kuhusu jalada lake, wakasema hili tunatayarisha mwishoni kabisa, ndipo nikawaambia nileteni jalada. Basi nikabadili jina la kitabu kuwa Mwana Mkuu wa Ibrahim, ambaye ni Mtume Mtukufu[saw] . Na kitabu kilichapishwa kwa jina hili.

Pindi kitabu kilipotoka matbaa baada ya kuchapishwa, siku hizo zilikuwa za maonyesho ya
Saba Saba. Kama wote wanajua maonyesho ya Saba Saba ni maonyesho makubwa, nchi nyingi zinayashiriki na kuleta bidhaa zao, watu hujaa kwa wingi kuona maonyesho na kununua bidhaa mbalimbali. Jumuiya pia inakuwa na banda katika maonyesho hayo kwa kuhubiri na kuuza vitabu. Banda linapangwa vizuri, picha za Jumuiya zinawekwa ukutani na watu wengi wanatembelea banda letu ili kununua vitabu vyetu na kujadili mambo ya dini. Wapinzani wetu pia hutembelea banda hilo na kuuliza maswali ambayo yanajibiwa barabara. Wakati Saba Saba ilikuwa imeshaanza, nilipigiwa simu na mkuu wa kiwanda cha uchapishaji kwamba “Mwana Mkuu wa Ibrahim” kipo tayari, lini nakala ziletwe misheni?

Nikawaambia vileteni katika banda letu ndani ya maonyesho ya Saba Saba. Basi vikaletwa kwenye banda letu.
Siku hiyo nilipokuwa naangalia baadhi ya mambo ya nje ya banda letu, nikaona mapadre wawili na sista mmoja wazungu wakizungumza karibu na banda letu. Kisha wakaingia banda letu, na kutoka. Tena mmoja wao akaingia ndani na kutoka, kisha wakaondoka.

Haraka nikaingia bandani na kuwauliza khuddam kuhusu mapadre hao. Nikaambiwa kuwa waliniambia walipoingia wote waliona kitabu cha Mwana Mkuu Wa Ibrahim na kukipekua pekua, kisha wakaondoka wote kisha mmoja wao alirudi na kununua kitabu hicho na kuondoka.

Baada ya Saba Saba kwisha, tuliporudi msikitini wakaja baadhi ya Waislam na Wakristo kutudai kitabu cha padre ili waweze kukilinganisha na kitabu chetu. Maulana anasema niliwaambia mnapaswa kupata kitabu chao kutoka duka lao ambamo vimejaa.
Wakaniambia hawana kitabu hicho kwenye duka lao. Nilishangaa sana. Nikafikiri pengine wameondoa kitabu chao baada ya jawabu lake. Jambo hili lilithibitika baada ya miezi sita, hivi kwamba Muahmadiyya mmoja Bw. R. B. Kazema aliyekuwa anapenda kuhubiri, na pia alikuwa mwandishi mzuri, aliyekuwa anaishi Ujiji uliopo mpakani mwa Tanzania na Zaire (ambayo siku hizi inaitwa Democratic Republic of Congo) aliniandikia barua kuwa Waislamu wasio Waahmadiyya wengi kutoka Zaire wananitembelea kwa ajili ya kununua vitabu vya Jamaat. Safari hii waliponijia waliweka kitabu cha Padre Anglars mbele yangu na kusema kwamba mapdare wamekisambaza sana nchini kwetu – jambo lililotusumbua na kuudhi sana. Tunaona Jumuiya yenu tu inaweza kupambana nao. Mwandike jawabu lake. Bwana Kazema aliandika kwamba niliweka Mwana Mkuu Wa Ibrahim mbele yao na kueleza kwamba tumeshaandaa jawabu lake. Wakafurahi sana, walikinunua na kuomba nakala zaidi. Basi nitumie nakala zake zingine. Maulana Jamil anasema nilimjibu kwamba nakala zake ziko karibu kwisha, nakuletea nakala chache. Utapelekewa baada ya chapa ya pili kutolewa. Anasema mara ya kwanza katika maisha yake aliona kwamba kwa kushindwa na kuogopa elimu ya hoja za Sayidina Ahmad as wapinzani si tu waliondoa kitabu chao madukani bali nchi nzima. Na elimu ya Sayidina Ahmad as iliwatawala vizuri.

Siku hizo hizo Maulana Muhammad Munawar, aliyekuwa Amiri na Mbashiri mkuu wa Kenya, alinipigia simu na kunijulisha kuwa baadhi ya wanafunzi Waislamu waliwapa kitabu chetu baadhi ya Wakristo, na wawili wao kwa kuvutika wamesilimu. Vitabu vyetu vilikuwa haviwezi kupelekwa Unguja. Lakini nilipewa taarifa kwamba kitabu chetu kiliwekwa katika maktaba ya Unguja. Anasema ni imani yangu kwamba wapinzani kwa fadhili ya Allah
walishindwa dhahiri shahiri kutokana na elimu ya hoja za Sayidina Ahmad as . Alhamdu Lillah

Khurram Shahzad

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE



UK> 08



MUHAJIRINA KATUTOKA

HABARI UK> 05

Ujumbe wa Huzuratba katika Jalsa Salana Tanzania

بسم الله الرحمٰن الرحيم

Ndugu Wanajumuiya wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya Tanzania.

Assalaam Alaikum Warahmatullah Wabarakaatuh.



Ninayo furaha kubwa ya kwamba mnafanya Jalsa Salana yenu ya 53 kwenye tarehe 27, 28 na 29 Septemba 2024.

Ni maombi yangu ya dhati kwamba, Mwenyezi Mungu aibariki Jalsa yenu kwa mafanikio makubwa na nyote mpate baraka kubwa na muongeze ujuzi na ufahamu wenu wa dini yetu ya Uislamu na mafundisho na mwongozo wa kipenzi chetu Mtume Muhammadsaw.

Kumbukeni, hili si tukio la kawaida la kidunia au tamasha. Masihi Aliyeahidiwaas alisema kama ifuatavyo:

'Lengo kuu la kukusanyika ni hili kwamba Wanachama waaminifu wa Jumuiya waweze kupata manufaa ya kidini na wakati huo huo waweze kupata zaidi maarifa, na kukua katika uhusiano wao na Mwenyezi Mungu. Faida moja ni kwamba kwa kukutana na marafiki mbalimbali, duara la udugu litapanuka na kutaimarisha mahusiano baina yao.'

(Asmani Faisla)

Kwa hiyo, tunapaswa kunufaika kikamilifu kutokana na mazingira matakatifu yanayozalishwa na mkusanyiko huu wa kipekee ili kuboresha utu wetu wa ndani na hivyo kutakasa hali yetu ya kikhulka ili tuweze kuimarisha imani yetu na kuongeza kiwango chetu cha Taqwa, yaani uchamungu na kukuza hofu ya kweli ya Mwenyezi Mungu ndani yetu.

Kwa hakika, Jalsa hii inatakiwa isababishe upole, wema na unyenyekevu kukua katika mioyo yetu. Inapaswa kutumika kama njia ya kuongeza mafungamano yetu ya upendo na udugu ndani ya Jumuiya, na kutuwezesha kuweka mfano bora wa sio tu kujaliana sisi wenyewe, bali pia kuangalia ustawi wa wanadamu wenzetu wenye uhitaji. Tunapaswa kustawisha unyenyekevu na upole katika utendaji na mwenendo wetu wa kila siku. Zaidi ya yote, tunapaswa kuendeleza bidii na shauku kwa ya huduma ya Uislamu na kujaribu kuanzisha uhusiano ulio hai na Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wetu.

Katika suala hili, Masihi Aliyeahidiwaas amesema:

HABARI UK> 08

NIDHAMU MPYA
Swahili Translation of
Nizaam-e-Nau
(THE NEW WORLD ORDER)

In the backdrop of the then prevailing ideologies of communism and capitalist democracy, the second successor of the Ahmadiyya Movement, Ḥaḍrat Mirzā Bashīruddīn Maḥmūd Aḥmadra, addressed this lecture to the Ahmadiyya Annual Gathering on December 28, 1942. The address answers the question, 'How does Ahmadiyyat, the True Islam, propose to deal with the grave problem of socio-economic inequality in the world?' The Ahmadiyya solution is the solution of Islam shaped under divine guidance for present needs by the Holy Founderas of the Ahmadiyya Movement.

The speaker examines and analyses the role played by different movements to alleviate poverty and sufferings, such as, Socialism, International Socialism, Marxism, Bolshevism, Nazism and Fascism and so on. The speaker also, explores the major religions of the world regarding the basic question 'social inequality a serious problem.'

Ḥaḍrat Mirza Ghulam Ahmad, the Promised Messiah and Mahdias, the founder of the Ahmadiyya Muslim Jamā'at, laid down the foundations of the New World Order, by initiating the scheme of *Waṣiyyat* based on Islamic teachings and under the Divine guidance in his book *Al-Waṣiyyat* written in 1905. Later in 1934 Ḥaḍrat Mirzā Bashīruddīn Maḥmūd Aḥmadra inaugurated *Taḥrīk-e-Jadīd* to prepare the ground for the full implementation of the New World Order of the institution of *Waṣiyyat*. In the present lecture he elaborates the aims and objectives of *Taḥrīk-e-Jadīd* and claims that the New World Order in all its aspects, economic, social and religious, as introduced by *Niẓām-e-Waṣiyyat,* will at the end prevail and a new and genuine revolution will take place.


ISBN 978-1-84880-523-1
9 781848 805231

NIDHAMU MPYA

NIDHAMU MPYA

HADHRAT MIRZA BASHIRUDDIN MAHMUD AHMAD
KHALIFATUL-MASIH II (MAY ALLAH BE PLEASED WITH HIM)

MIRZA BASHIRUDDIN MAHMUD AHMADra



Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 4,000/=.

Je, Wajua?

Gravity inategemea ukubwa na uzito wa kitu. Mfano, uzito na ukubwa wa dunia hufanya gravity ya dunia kuwa ilivyo na jua vivyo hivyo.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com